PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

PPAA
Toleo Na: 06 Julai - Septemba 2025

# BULLETIN

UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## PPAA yatoa elimu ya matumizi ya moduli Sabasaba, Nanenane:

## ■ Yabadilishana uzoefu matumizi ya Moduli nchini Kosovo

Mpendwa msomaji wa Jarida hili karibu tena ujisomee Toleo la Sita (06) la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) "PPAA Bulletin". Jarida hili hutumika kama njia mojawapo ya Mawasiliano ya Kimkakati ya PPAA kuuhabarisha umma kuhusu majukumu na shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu. Jarida hili ni mwendelezo wa majarida mengine yaliyopita yanayokuhabarisha kuhusu shughuli za PPAA kwa kipindi cha miezi mitatu.

Ninayo furaha kukuletea Toleo la Sita la PPAA Bulletin kwa kipindi kingine tena cha miezi mitatu (Julai – Septemba, 2025), kwa lengo la kukuhabarisha juu ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi tajwa.

Mbali na kutekeleza jukumu lake la msingi la kushughulikia malalamiko na rufaa zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi tajwa, PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi wa umma na umma kwa ujumla katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarufu kama Sabasaba na Maonesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Nanenane pamoja na kufanya ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki nchini Kosovo.

Aidha, katika toleo hili, tumekuandalia habari mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya PPAA katika kufikia malengo iliyokusudia kwa kipindi tajwa.

Karibu usome jarida hili ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli mbalimbali ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Julai – Septemba, 2025) na kuendeleza ushirikiano imara katika utoaji rufaa kwa ufanisi, wakati na kwa haki kwenye sekta ya ununuzi wa umma.

***#Kazi na Utu, Tunasonga Mbele.***

# PPAA, PRB na PPRC zabadilishana uzoefu mifumo ya ununuzi wa umma

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imebadilishana uzoefu wa matumizi ya mifumo ya kusimamia rufaa katika ununuzi wa umma na Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB) pamoja na Tume ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC) za nchini Kosovo.**

Ubadilishanaji uzoefu wa namna ya kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki ulifanyika wakati wa ziara ya mafunzo ya ujumbe wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), ulioongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Jaji Mstaafu Awadh Bawazir, walipokutana na Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB).

*> Habari kamili ukurasa wa 3*




*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Mhe. Jaji Mstaafu Awadh Bawazir (kushoto) akichangia jambo wakati ujumbe wa PPAA ulipokutana na Tume ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC) katika ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna taasisi za ununuzi wa umma nchini Kosovo zinavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma.*


BULLETIN
PPAA, PRB na PPRC zabadilishana uzoefu mifumo ya ununuzi wa umma

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Florida Mapunda

**Mhariri**
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

**Wajumbe**
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga

**Katibu**
Nelson Kessy

**Mawasiliano:**
Katibu Mtendaji
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz

# PPAA yatoa rai wazabuni kutumia Moduli Kuwasilisha Rufaa


*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akiongea na waandishi wa habari katika banda la mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam Julai 2025.*

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetoa rai kwa wazabuni kutumia Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST ili kuokoa muda na gharama zisizo na ulazima.**

Rai hiyo imetolewa na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando alipoongea na waandishi wa habari katika banda la mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarifi Sabasaba jijini Dar es Salaam, Julai 2025.

Bw. Sando amewasihi wazabuni kuitika wito wa serikali wa kutumia mfumo wa NeST ambapo ndani ya mfumo huo kuna moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa, hivyo watumie fursa hiyo kuwasilisha malalamiko na rufaa zao.

"Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST ni suluhisho kwa wazabuni katika kuwasilisha rufaa pindi wanapokuwa hawajaridhishwa na mchakato wa ununuzi wa umma katika zabuni walizoshiriki," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando ameongeza kuwa baada ya matumizi ya moduli kuanza rasmi Februari 2025 mzabuni halazimiki kufika ofisi za Mamlaka ya Rufani kuwasilisha rufaa, badala yake atumie moduli kuwasilisha rufaa husika kupitia mfumo wa NeST.

Aidha, Bw. Sando ameongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2025/26 PPAA inatarajia kuanza kusikiliza mashauri kwa njia ya mtandao ili kurahisisha zaidi usikilizaji wa rufaa pale itakapoonekana kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando amesema moduli ina faida nyingi hususan kuokoa muda na grahama, imerahisisha upatikanaji wa nyaraka, kutunza kumbukumbu pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Katika kuhakikisha matumizi ya moduli yanawafikia wazabuni wengi kwa wakati uliokusudiwa, PPAA imeshatoa mafunzo ya namna ya kuwasilisha malalamiko na rufaa kwa njia ya kieletroniki katika kanda mbalimbali ambapo mpaka sasa Kanda ya Pwani, ya Ziwa, ya Kaskazini, ya Nyanda za Juu Kusini na ya Kati zimepatiwa mafunzo.

Aidha, katika mafunzo hayo PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 873 na wakuu wa idara/vitengo vya ununuzi na sheria wapatao 1,588 kutoka katika taasisi nunuzi 500.



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akiongea na baadhi ya watumishi wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) alipotembelea banda la Wizara ya Fedha kwenye Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam, Julai 2025.*




*Rais wa Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB), Bw. Isa Hasani akiueleza ujumbe wa PPAA historia ya PRB na jinsi inavyoshughulikia migogoro kielektroniki katika sekta ya ununuzi wa umma nchini Kosovo wakati wa ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna taasisi za ununuzi wa umma nchini Kosovo zinavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma.*

# PPAA, PRB na PPRC zabadilishana uzoefu mifumo ya ununuzi wa umma

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imebadilishana uzoefu wa matumizi ya mifumo ya kusimamia rufaa katika ununuzi wa umma na Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB) pamoja na Tume ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC) za nchini Kosovo.**

Ubadilishanaji uzoefu wa namna ya kushughulikia malalamiko na rufaa kieletroniki ulifanyika wakati wa ziara ya mafunzo ya ujumbe wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), ulioongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Jaji Mstaafu Awadh Bawazir, walipokutana na Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB).

Akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani Jaji Mstaafu Mhe. Awadh Bawazir alisema lengo la ziara hiyo ni kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna taasisi za ununuzi wa umma nchini Kosovo zinavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma hususan namna ya kushughulikia malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma kieletroniki.

"Ni imani yangu kuwa kupitia ziara hii tutajifunza na kubadilishana uzoefu wa kutumia mifumo ya tehama katika kushughulikia rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma na kutuwezesha kuisaidia Serikali kupata thamani halisi ya fedha katika miradi inayotekelezwa na itakayotekelezwa," amesema Mhe. Bawazir.

Ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kujenga mfumo imara wa kusimamia ununuzi wa umma nchini (NeST).

Akielezea kuhusu mfumo wa Ununuzi wa Umma nchini Tanzania katika kikao hicho, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando ameeleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeiwezesha PPAA kujenga Moduli ya kupokea na kushughulikia rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma kieletroniki, ambapo hivi sasa malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi huwasilishwa kupitia moduli hiyo (Complaints and Appeal Management Module) inayopatikana katika mfumo wa NeST.

"Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST inafaida nyingi kwa wazabuni, taasisi nunuzi na PPAA. Kwa mfano faida mojawapo Moduli hii ina okoa muda na gharama kwa mzabuni kwa kuwa hatalazimika kusafiri ili aweze kuwasilisha malalamiko au rufaa yake PPAA," ameeleza Bw. Sando.

Aidha, Moduli hii inaokoa muda, gharama na kuongeza uwazi na uwajibikaji.

Kwa upande wake Rais wa Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB), Bw. Isa Hasani amesema kuwa PRB ni taasisi huru yenye jukumu la kupitia malalamiko yanatokana




*Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Mhe. Jaji Mstaafu Awadh Bawazir akichangia jambo wakati ujumbe wa PPAA ulipokutana na Tume ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC) katika ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna taasisi za ununuzi wa umma nchini Kosovo zinavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma.*

# PPAA, PRB na PPRC zabadilishana uzoefu mifumo ya Ununuzi wa Umma

na michakato ya ununuzi wa umma.

"Bodi hii ni chombo muhimu katika kuhakikisha kuwa taratibu za ununuzi zinafanyika kwa haki na uwazi, kwa kushughulikia migogoro kati ya mamlaka za manunuzi na waendeshaji wa kiuchumi (wazabuni, watoa huduma, na wakandarasi)," amesema Bw. Hasani.

Ameongeza: "Mifumo ya ununuzi wa umma kieletroniki imetuwezesha kushughulikia rufaa nyingi kwa wakati ambapo tangu mwaka 2019 hadi 2025 tumeweza kupokea na kushughulikia kieletroniki rufaa 7,984 zilizowasilishwa na wazabuni kuhusiana na michakato mbalimbali ya ununuzi wa umma," alieleza Bw. Hasani.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC), Bw. Avni Sahiti ameipongeza Tanzania kwa kuwa na mfumo rafiki wa kusimamia ununuzi wa Umma na kuongeza kuwa ziara ya ujumbe wa PPAA nchini Kosovo imelenga kuimarisha ushirikiano wa pande mbili na kuhamasisha ubadilishanaji wa mbinu bora katika ununuzi wa umma.

Katika kikao hicho, Bw. Sahiti na Bi. Fidane Spahija Gjikolli, waliwasilisha muhtasari wa muundo wa PPRC, mfumo wa udhibiti wa sheria na taratibu za kiutendaji.  Aidha, mtaalamu wa tehama, Bw. Gazmend Gashi, alitoa wasilisho kuhusu mchakato wa kuwasilisha malalamiko kupitia mfumo wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (E-Procurement), akisisitiza hatua zilizopigwa na Kosovo katika uwazi wa kidijiti na ufanisi wa mifumo.

Kadhalika, ujumbe wa PPAA ulifanya ziara katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAO) pamoja na Idara ya Uratibu wa Ukaguzi wa Ndani (CHDIA).  Hizi ofisi mbili zinafanya ukaguzi wa masuala mbalimbali ikiwemo ununuzi wa umma.

Ujumbe wa PPAA umeonesha hamasa kubwa juu ya mageuzi ya ununuzi wa umma nchini Kosovo pamoja na mifumo ya kuhakikisha uwajibikaji na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.



*Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando akichangia jambo wakati ujumbe wa PPAA ulipokutana na wajumbe wa Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB) hawapo pichani, katika ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna taasisi za ununuzi wa umma nchini Kosovo zinavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma.*




*Kikao kazi baina ya ujumbe kutoka PPAA ulipokutana na Tume ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC) wakati wa ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna taasisi za ununuzi wa umma nchini Kosovo zinavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma.*



*Picha ya ujumbe kutoka PPAA na ujumbe kutoka Bodi ya Mapitio ya Ununuzi (PRB) baada ya kumaaliza kikao kazi cha kubadilishana uzoefu wa namna taasisi za ununuzi wa umma nchini Kosovo zinavyotekeleza majukumu yake katika sekta ya ununuzi wa umma.*

# PPAA yafanya ziara ya kikazi nchini Kosovo




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Kosovo, Bw. Ilir Muçaj akijadili jambo na Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando baada ya ujumbe wa PPAA kuwasili jijini Prishtina kwa ziara ya kikazi Julai, 2025.*

**Ujumbe wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ukiongozwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Mhe. Awadh Bawazir umefanya ziara jijini Prishtina nchini Kosovo kwa ziara ya kikazi ya siku tano kuanzia tarehe 14 – 18 Julai, 2025.**

Katika ziara hiyo Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani ameambatana na wajumbe wa mamlaka ya rufani, Kamishna wa Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, Mkurugenzi wa Mipango Wizara ya Fedha, Bw. Moses Dulle pamoja na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya PPAA.

Mwenyekiti wa Ujumbe huo, Jaji Mstaafu Mhe. Awadh Bawazir ameeleza lengo la ziara hiyo ni kujifunza na kupata uzoefu wa taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma na mnyororo wa ununuzi wa umma hususan katika masuala ya ununuzi wa umma, uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroni nchini Kosovo.

Baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Prishtina, ujumbe wa PPAA ulipokewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Kosovo, Bw. Ilir Muçaj.

Ujumbe huo ukiwa nchini Kosovo ulitembelea Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PRD), Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC), Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAO), pamoja na Idara ya Uratibu wa Ukaguzi wa Ndani (CHDIA).



*Ujumbe wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ukiongozwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Mhe. Jaji Mstaafu Awadh Bawazir (kushoto) ukijadili jambo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Kosovo, Bw. Ilir Muçaj (Katikati) baada ya ujumbe wa PPAA kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Adem Jashari Prishtina kwa ziara ya kikazi mwezi Julai 2025. Kulia aliyevaa skafu ya bendera ya Tanzania ni Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando.*

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 06 Julai -Septemba 2025

# Prof. Pallangyo aipongeza PPAA kuanza matumizi ya Moduli



*Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Profesa William Pallangyo akipata maelezo kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa NeST kutoka kwa Afisa Mwandamizi wa PPAA, Bw. Stanley Jackson wakati wa Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, Julai 2025 jijini Dar es Salaam.*

**Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Profesa William Pallangyo ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika mfumo wa NeST.**

Prof. Pallangyo ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la PPAA katika Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba jijini Dar es Salaam, Julai 2025.

Akiongea kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, Afisa Mwandamizi wa mamlaka hiyo, Bw. Stanley Jackson amesema Mamlaka ya Rufani imefanya mapinduzi makubwa ya teknolojia kwa kujenga Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia mfumo wa NesT ambapo moduli hiyo imerahisisha zoezi la kuwasilisha malalamiko na rufaa kwa wazabuni na Taasisi Nunuzi.

"Awali kabla ya ujenzi wa moduli, wazabuni walikuwa wanalazimika kufika katika ofisi za PPAA kuwasilisha malalamiko yao, ila sasa baada ya kujengwa kwa moduli mzabuni anawasilisha malalamiko na rufaa kieletroniki jambo linalorahisisha na kuokoa muda na gharama kwa wazabuni na Taasisi Nunuzi," amesema Bw. Jackson.

Februari, 2025 Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ilizindua rasmi matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Kieletroniki (NeST) jijini Mwanza wakati wa mafunzo ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika mfumo wa NeST.

Hadi sasa PPAA imefanikiwa kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kieletroniki katika kanda ya Pwani, ya Ziwa, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati zimepatiwa mafunzo.

Aidha, katika mafunzo hayo PPAA imefanikiwa kutoa elimu kwa wazabuni 873 na wakuu wa idara/vitengo vya ununuzi na sheria wapatao 1,588 kutoka katika taasisi nunuzi 500.



*Sehemu ya wadau waliotembelea Banda la PPAA kupata elimu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na mamlaka hiyo wakati wa Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, Julai 2025 jijini Dar es Salaam.*




*Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda hilo kwenye Maonesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma, Agosti 2025.*

# Bi. Omolo aipa kongole PPAA kuwanoa wazabuni matumizi Moduli ya Kuwasilisha Rufaa




*Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo akizungumza na watumishi wa PPAA (Hawapo pichani) alipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma, Agosti 2025.*

**Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, ameipongeza Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kuendelea vyema kutoa mafunzo kwa wazabuni na taasisi nunuzi kuhusu mafunzo juu ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika mfumo wa NeST.**

Bi. Omolo ametoa pongezi hizo alipotembelea Banda la PPAA kwenye Maonesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Nanenane yanayofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma na kujionea huduma zinazotolewa na PPAA katika maonesho hayo.

Pamoja na mambo mengine, Bi. Omolo ameitaka PPAA kuendelea kutoa mafunzo hayo kwa wadau wengi zaidi hususan katika ngazi za mikoa na wilaya ili kutoa fursa kwa wadau wengi zaidi kupata uelewa wa matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa katika Mfumo wa NeST.

Maonesho ya mwaka huu yanaongozwa na kaulimbiu: "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi 2025".




*Baadhi ya wadau wa ununuzi wa umma wakipewa maelezo na Maafisa wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) walipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma, Agosti 2025.*

# PPAA yatoa elimu kwa wazabuni, umma maonesho ya nanenane

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imeshiriki Maonesho ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma kutoa elimu kuhusu ununuzi wa umma kwa wazabuni, hususan elimu kuhusu Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.**

Akiongea kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, Bw. Nelson Kessy amesema PPAA imejipanga kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi wa umma na wananchi kwa ujumla ili kutoa wigo mpana zaidi kwa wazabuni na wadau wa sekta hiyo.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Kessy amewasihi wadau wa ununuzi na wananchi kwa ujumla kutembelea Banda la PPAA linalopatikana ndani ya Banda la Wizara ya Fedha katika viwanja vya Nzuguni, Dodoma kujifunza zaidi.

Maonesho ya Nanenane Kitaifa yalianza Agosti Mosi, 2025 na yalifungwa rasmi tarehe 08 Agosti, 2025 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza katika kilele cha maonesho hayo ya Nanenane, Rais Dkt. Samia amesema miradi ya umwagiliaji iliyokamilika na inayoendelea kutekelezwa inapaswa kusimamiwa kwa viwango bora ili kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji na kukuza tija ya mavuno.

Kadhalika maonesho hayo yalifunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango tarehe 01 Agosti, 2025 katika hivyo jijini Dodoma.

Akifungua Maonesho hayo, Dkt. Mpango ametoa rai kwa viongozi kutambua wajibu wa kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 na Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo inayolenga kuongeza kasi ya ukuaji wa kilimo hadi kufikia asilimia 10 kwa mwaka ifikapo 2030.

Wizara ya Maji, taasisi na mamlaka zake zimeshiriki katika maonesho hayo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya shughuli zinazofanywa na mamlaka na taasisi za sekta ya maji katika kuhakikisha lengo la huduma ya majisafi na usafi wa mazingira zinawafikia wananchi.

Maonesho haya kwa mwaka 2025 yamebeba kauli mbiu isemayo: “Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi 2025”.




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), Profesa Geraldine Rashel akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda hilo kwenye Maonesho ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni jijini Dodoma, Agosti 2025.*

# Muda watengua rufaa dhidi ya Wizara ya Afya

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetupilia mbali rufaa iliyowasilishwa dhidi ya Wizara ya Afya kutokana na kuisha kwa muda wa uhai wa zabuni, na kuamuru kila upande kujigharamia wenyewe.**

Uamuzi huo umeotolewa Agosti 2025 na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Awadh Bawazir kwenye rufaa iliyowasilishwa na Kampuni ya Softmed Company Ltd dhidi ya Wizara ya Afya kuhusu zabuni ya kutoa huduma za ushauri kwa ajili ya kusaidia na kudumisha moduli za HIV kwenye mfumo wa kijamii uliojumuishwa - NASHCOP.

Mlalamikaji ameeleza kuwa zabuni hiyo ilitangazwa tarehe 30 Julai 2024 na ufunguzi wake ulifanyika tarehe 13 Agosti 2024 ambapo muda wa uhalali wa zabuni hiyo ulikuwa siku 120 kama ilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni.

Aidha, mlalamikaji alieleza kuwa muda wa uhalali wa zabuni unahesabiwa kuanzia siku ya ufunguzi wa zabuni yaani kuanzia tarehe 13 Agosti 2024, ambapo muda wa siku 120 wa uhalali wa zabuni uliisha tarehe 13 Desemba 2024.



Alisisitiza kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma inataka muda wa uhai wa zabuni uainishwe ndani ya nyaraka za zabuni. Kwa kuwa kipindi kilichobainishwa katika Ombi la Mapendekezo (RFP) kilikuwa siku 120, Wizara ya Afya ililazimika kumaliza mchakato wa zabuni ndani ya muda huo. Kinyume chake, Wizara ya Afya iliendelea na mchakato wa zabuni hadi tarehe 24 Juni 2025 ilipotoa taarifa ya kusudio la kutoa zabuni (Notice of Intention to award the Tender) kwa mzabuni mshindi.

Mlalamikaji aliongeza kuwa, kwa kuwa tayari muda wa uhai wa zabuni ulikuwa umeisha hatua zozote zilizochukuliwa na Wizara ya Afya ni batili kisheria. Hivyo hakukuwa na zabuni halali ya kuamuliwa na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma.

Kwa upande wake, Wizara ya Afya ilianza kwa kueleza kuwa Ombi la Mapendekezo (RFP) iliainisha muda wa uhai wa zabuni kuwa siku 120, ambazo zilipaswa kuhesabiwa kuanzia tarehe ya ufunguzi wa zabuni yaani tarehe 13 Agosti 2024. Kwa hesabu hiyo, muda huo ulimalizika Desemba 2024.

Wakili wa Serikali alieleza kuwa kabla ya muda wa uhai wa zabuni kumalizika, Wizara ya Afya ilifanya tathmini ya zabuni zilizopokelewa kuanzia tarehe 19 hadi 27 Agosti 2024. Hata hivyo, kabla ya kukamilisha michakato ya ndani, walikumbana na changamoto kwenye mfumo wa NeST, ambapo baadhi ya taarifa za zabuni zilikuwa zikifutika mara kwa mara. Kutokana na changamoto hiyo, haikuwezekana kukamilisha mchakato wa zabuni ndani ya muda uliopangwa wa uhai wa zabuni.

Baada ya kubaini changamoto hizo, Wizara ya Afya iliwaomba wazabuni wote kuongeza muda wa uhai wa zabuni kwa siku 120 kupitia barua ya tarehe 29 Novemba 2024, iliyotumwa kwa njia ya barua pepe kwa wazabuni wote isipokuwa mlalamikaji (Softmed), ambaye zabuni yake ilienguliwa katika hatua ya awali ya tathmini.

Aidha, Wizara ya Afya ilieleza kuwa hata muda wa nyongeza huo haukukamilisha mchakato wa zabuni, hivyo waliomba tena nyongeza ya siku 40 kupitia barua ya tarehe 28 Machi 2025. Muda wa pili wa nyongeza uliisha tarehe 10 Mei 2025 bila mchakato wa zabuni kukamilika. Kwa msingi huo, Wizara ya Afya ilihitimisha kuwa zabuni inayolalamikiwa ilikuwa imekwisha muda wake.

Katika kikao cha usikilizwaji wa shauri hilo, Mamlaka ya Rufani iliitaka Wizara ya Afya ibainishe iwapo wazabuni walikubali ombi la kuongeza muda wa uhai wa zabuni.

Aidha, Wizara ilieleza kuwa wazabuni walikubali ombi hilo, lakini hawakuweza kuwasilisha barua za uthibitisho kutoka kwa wazabuni husika kwa kuwa walikuwa wamehamia katika ofisi mpya Mtumba - Dodoma, jambo lililosababisha ugumu katika kupata nyaraka zote muhimu za zabuni hiyo.

Wakili wa Serikali alikamilisha hoja zake kwa kusisitiza kuwa kumbukumbu zinaonesha wazi kuwa zabuni ilikwisha muda wake mwezi Mei 2025, na hivyo hakuna zabuni halali ambayo Mamlaka ya Rufani inaweza kuizingatia katika rufaa hiyo.

Mamlaka ya Rufani katika kuamua msingi wa rufaa hiyo, ilizingatia kuwa pande zote mbili zilikuwa zimekubaliana kuwa muda wa uhai wa zabuni ulikuwa siku 120 na tayari ulikuwa umeisha. Kwa kuwa Wizara ya Afya iliendeleza mchakato wa zabuni baada ya muda huo kuisha, na baadaye mlalamikaji kuwasilisha rufaa, PPAA iliona ni vyema kuzifahamisha pande zote juu ya matakwa ya kisheria kuhusu muda wa uhai wa zabuni.

Sheria inaitaka taasisi nunuzi ihakikishe kuwa wazabuni wanaweka zabuni na dhamana za zabuni kuwa hai kwa muda uliobainishwa kwenye nyaraka za zabuni, muda ambao unatosha kukamilisha hatua za kulinganisha na kutathmini zabuni, kupata idhini ya mapendekezo, kutoa taarifa ya kusudio la kutoa tuzo na kusaini mkataba wakati zabuni na dhamana zikiwa bado hai.

PPAA ilipitia Ombi la Mapendekezo (RFP) na kubaini kuwa muda wa uhai wa zabuni ulioainishwa ulikuwa siku 120. Kumbukumbu ya rufaa ilionesha kuwa ufunguzi wa zabuni ulifanyika tarehe 13 Agosti 2024, hivyo muda wa uhai wa zabuni ulimalizika rasmi tarehe 11 Desemba 2024.

Wakati wa usikilizwaji, Wizara ya Afya ilidai kuwa kabla ya muda wa uhai wa zabuni kumalizika, iliwaandikia wazabuni barua ya tarehe 29 Novemba 2024 ikiomba kuongeza muda kwa siku 120. Aidha, ilidai pia kuwa iliomba nyongeza nyingine ya siku 40 kupitia barua ya tarehe 28 Machi 2025. Hata hivyo, Wizara ilishindwa kuthibitisha iwapo maombi hayo yaliwasilishwa kwa wazabuni na kama waliyakubali.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, ombi la kuongeza muda wa uhai linaweza kufanywa tu katika mazingira ya kipekee na lazima lifanywe kabla ya muda wa awali kuisha. Pia, mzabuni ana haki ya kukataa bila kupoteza dhamana yake, na kukubalika au kukataliwa kwa ombi hilo lazima kuwasiliana kwa maandishi.

PPAA ilibaini kuwa, pamoja na madai ya Wizara, hakukuwa na ushahidi wowote ulioonesha kuwa wazabuni walikubali nyongeza hiyo. Kwa kuwa Wizara ilishindwa kuthibitisha, kuwa iliwaomba wazabuni kuongeza uhai wa zabuni kabla ya muda wa awali kuisha.

PPAA ilihitimisha kuwa hatua zote zilizochukuliwa na Wizara baada ya kuisha kwa muda wa uhai wa zabuni tarehe 11 Desemba 2024 ikiwemo kutoa taarifa ya kusudio la kutoa zabuni tarehe 24 Juni 2025 ni batili kwa kuwa ulikiuka matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Kwa msingi huo, PPAA ilifuta mchakato wa zabuni kutokana na kuisha kwa muda wa uhai wa zabuni. PPAA ilitupa rufaa dhidi ya Wizara ya Afya kwa sababu ya kuisha kwa muda wa uhai wa zabuni na kuamuru kila upande kujigharamia wenyewe.

# Rufaa dhidi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yakosa mashiko, yatupiliwa mbali

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetupilia mbali rufaa iliyokatwa dhidi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kukosa mashiko, na kuiruhusu Wizara kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia sheria.**

Uamuzi huo ulitolewa mwezi Agosti 2025 mbele ya Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Mhe. Awadh Bawazir, juu ya rufaa iliyowasilishwa na Kampuni ya Technowise Ltd dhidi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuhusiana na zabuni ya Utoaji wa Huduma za Ushauri wa Kufanya Utafiti wa Uwezekano wa Uendelezaji wa Miji Mahiri (Smart Cities) katika Jiji la Dodoma, Arusha na Mbeya.

Mlalamikaji alipinga kuondolewa kwa zabuni yake kwa misingi mitatu ambayo ni: matumizi yasiyo sahihi ya njia ya QCBS, mkanganyiko katika vigezo vya tathmini ya kifedha, na kushindwa kuweka wazi matokeo ya tathmini ya mapendekezo ya kiufundi kama ilivyotakiwa kwenye nyaraka za zabuni.



Kuhusu matumizi yasiyo sahihi ya njia ya QCBS, mlalamikaji alieleza kuwa nyaraka za Ombi la Pendekezo (RFP) zilieleza wazi kuwa njia ya kuchagua zabuni ni QCBS. Aidha, alibainisha kuwa nyaraka za zabuni zilieleza kuwa uzito wa tathmini ya mapendekezo ya kiufundi ni asilimia 80 na ya kifedha ni asilimia 20. Aliongeza kuwa nyaraka hizo zilitaka mapendekezo ya kifedha yapimwe kwa kuzingatia bei ya chini zaidi na kisha kuunganishwa na alama za kiufundi ili kubaini mshindi wa zabuni.

Zaidi ya hayo, mlalamikaji aliwasilisha kwamba kwa kuwa taarifa ya kusudio la kutoa Zabuni (Notice of Intention to Award) ilionyesha kuwa pendekezo lake lilikataliwa kwa sababu halikuwa na bei ya chini zaidi katika tathmini ya kifedha, ikimaanisha kwamba uamuzi wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa kutoa zabuni ulitokana tu na pendekezo la kifedha, jambo linalopingana na njia ya QCBS. Alisema kuwa chini ya njia ya QCBS, bei peke yake haiwezi kuwa kigezo cha kuamua mshindi wa mkataba, kwani vigezo vingine vya kiufundi vinapaswa kuzingatiwa kabla ya kuangalia bei.

Kuhusiana na vigezo vya tathmini ya kifedha, wakati wa usikilizwaji wa shauri, PPAA ilimwomba mlalamikaji kufafanua iwapo aliwahi kuomba ufafanuzi kabla ya kuwasilisha zabuni yake. Alieleza kuwa hakuomba ufafanuzi kwa kuwa kigezo cha tathmini ya kifedha kilieleza wazi kuwa alama hazingetumika. Hivyo basi, alitarajia kuwa alama hazingeweza kutumika kama ilivyobainishwa katika nyaraka za zabuni.

Mlalamikaji alieleza kuwa nyaraka za zabuni zilihitaji wazabuni kufahamishwa matokeo ya tathmini ya kiufundi kabla ya kuendelea na ufunguaji wa mapendekezo ya kifedha. Alibainisha kuwa katika zabuni husika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari haikutoa matokeo ya tathmini ya kiufundi kama ilivyotakiwa na Nyaraka ya zabuni. Aidha, alidai kuwa Wizara ilivunja kanuni ya uwazi kama inavyotolewa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Mlalamikaji aliongeza kuwa kushindwa kwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutoa matokeo ya tathmini ya kiufundi kuliibua mashaka kuhusu namna kigezo cha watumishi muhimu (key personnel) kilivyopimwa. Alieleza kuwa nyaraka za zabuni zilieleza wazi kuwa alama zilizotengwa kwa kigezo cha watumishi muhimu ni 40. Aidha, alibainisha kuwa kigezo cha uzoefu katika eneo husika na lugha kilitengewa asilimia 10, wakati kigezo cha sifa za jumla kilitengewa asilimia 30, na kufanya jumla ya asilimia 40, na kuacha asilimia 60. Alisisitiza kuwa baada ya makadirio kufanywa, asilimia 40 iliyotengwa ilitafsiriwa kuwa alama 24 pekee kati ya jumla ya alama 40. Hivyo basi, alidai kuwa mchakato wa tathmini ulikuwa na kasoro kwa kuwa asilimia 60 zilizobaki hazikutengewa kigezo chochote.

Aidha, Technowise Ltd ilieleza kuwa wakati wa kuandaa zabuni yake, aliambatisha nyaraka zote zilizohitajika, na zabuni hiyo iliwasilishwa kwa mafanikio kupitia mfumo wa NeST. Hata hivyo, baada ya kupita siku chache tangu tarehe ya kuwasilisha, alibaini kuwa nyaraka iliyoonyesha njia za namna ya utekelezaji na ubora wa jumla wa pendekezo haikuonekana ingawa ilikuwa imewasilishwa. Aliongeza kuwa ana mashaka iwapo nyaraka hiyo iliyopotea ilizingatiwa na kamati ya tathmini wakati wa kufanya tathmini na iwapo iliwekewa alama stahiki. Kutokana na hali hiyo, aliiomba Mamlaka ya Rufani kuchunguza upya mchakato wa zabuni ili kubaini iwapo ulifanyika kwa mujibu wa sheria.

Kwa upande wake, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilieleza kwamba katika rufaa hiyo, mlalamikaji aliwasilisha misingi mitatu pekee ya rufaa, lakini katika mawasilisho ya mdomo aliongeza hoja mbili mpya ambazo hazikuwemo katika rufaa ya awali, ambazo ni: dosari katika mgao wa alama asilimia 40 kwa kigezo cha watumishi muhimu, na madai ya nyaraka iliyowasilishwa katika mfumo wa NeST kuhusu njia ya namna ya utekelezaji na ubora wa pendekezo kupotea.

Wakili wa Serikali kutoka Wizarani alieleza kuwa kanuni ya msingi ya sheria inazitaka pande zote kujibu hoja zilizowasilishwa kwa maandishi. Pande haziruhusiwi kuibua hoja mpya wakati wa usikilizaji ambapo hazikuwemo awali katika maandishi. Kwa kuunga mkono msimamo huu, aliomba Mamlaka ya Rufani isiingilie au kuzingatia hoja mpya wakati wa kuamua rufaa.

Wakili wa Serikali alieleza kuwa kuhusiana na kasoro katika mgao wa alama asilimia 40 kwa kigezo cha watumishi muhimu, Sheria ya Ununuzi wa Umma inataka mzabuni asome kwa makini nyaraka za zabuni na kuamua iwapo anaweza kutimiza masharti ya kiufundi, kifedha, na ya mkataba kabla ya kuwasilisha pendekezo lake. Aliongeza kuwa sheria hiyo inamtaka mzabuni kupitia kwa umakini nyaraka za zabuni na kubaini kama kuna ukosefu, upungufu, au mkinzano wa ndani, au masharti mengine yasiyo wazi, yanayoonekana kuwa na ubaguzi au kizuizi. Aidha, iwapo mzabuni atagundua ukosefu wa uwazi au kasoro katika vigezo vilivyotolewa, anahitaji kuomba ufafanuzi kutoka kwa taasisi nunuzi. Hata hivyo, kwa kuwa mlalamikaji alishiriki katika

>> Inaendelea Ukrasa wa 11

# Rufaa dhidi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yakosa mashiko, yatupiliwa mbali

zabuni hii bila kuomba ufafanuzi, inaashiria kuwa alikubali kushikamana na masharti ya nyaraka za zabuni.

Kuhusu kasoro katika mgao wa alama asilimia 40, Wakili wa Serikali alieleza kuwa kigezo hicho kilikuwa na vigezo vidogo vitatu, vyote vilifanyiwa tathmini kulingana na mahitaji yaliyotolewa katika nyaraka za zabuni. Alibainisha kuwa hakukuwa na kasoro yoyote kama ilivyodaiwa na mlalamikaji; kwa hivyo, aliomba Mamlaka ya Rufani kutozingatia hoja hiyo.

Mbali na hoja za mlalamikaji zilizotolewa wakati wa usikilizwaji, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilisema kuwa msingi wa kwanza wa rufaa wa zabuni iliwasilishwa kupitia mfumo wa NeST na ilizingatia vigezo vilivyotolewa katika nyaraka ya zabuni. Aidha, Wakili wa Serikali aliongeza kuwa mchakato wa tathmini ulitekelezwa kwa kuzingatia kanuni za ununuzi wa umma za uadilifu, ushindani, uwajibikaji, uchumi, ufanisi, uwazi, thamani ya fedha na ushiriki wa haki kwa wazabuni wote kama inavyoelekezwa kwenye Sheria ya ununuzi wa Umma.



Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliongeza kuwa sababu ya kuondolewa kwa zabuni ya mlalamikaji, kama ilivyooneshwa katika taarifa ya kusudio la kutoa zabuni (Notice of Intention to Award), siyo sababu halisi ya kuondolewa kwake. Mfumo wa NeST ulitoa sababu ya jumla badala ya sababu halisi ya kuondolewa kwa zabuni ya mlalamikaji.

Kuhusiana na msingi wa pili wa rufaa kwamba kulikuwa na mkinzano katika vigezo vya tathmini ya kifedha, Wakili wa Serikali alieleza kuwa tathmini ya kifedha ilifanywa kwa mujibu wa njia ya hesabu iliyoainishwa katika nyaraka za zabuni. Baada ya kumalizika kwa mchakato wa tathmini ya kifedha, alama za kiufundi na kifedha ziliunganishwa. Wakili wa Serikali alibainisha kuwa uzito wa kuchanganya alama za kiufundi na kifedha ulitekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hivyo basi, hoja iliyowasilishwa na mlalamikaji kwamba vigezo vya tathmini ya kifedha vilikuwa na ukosefu wa uwazi au mchakato wa tathmini ulifanywa kinyume na sheria, haina msingi na inapaswa kupuuzwa.

Msingi wa tatu ulihusu ufafanuzi wa matokeo ya tathmini ya kiufundi, Wizara ilibainisha kuwa matokeo hayo hayawezi kufahamishwa kwa mlalamikaji kupitia mfumo wa NeST kwani mfumo huo haujatengenezwa kuruhusu taasisi nunuzi kutoa matokeo ya tathmini ya kiufundi kwa wazabuni kabla ya kwenda kwenye uchambuzi wa kifedha. NeST bado ipo katika hatua za ujenzi na baadhi ya vipengele bado havipo. Aidha, alisisitiza kuwa, kwa kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma inataka mchakato wote wa zabuni ufanyike kupitia NeST, Wizara haingeweza kufahamisha matokeo hayo nje ya mfumo, kwani ingekuwa kinyume na sheria.

Katika kuamua msingi wa rufaa hiyo, Mamlaka ya Rufani ilikagua hoja za pande zote mbili kuhusu msingi wa kwanza wa rufaa. Hoja ya mlalamikaji kwamba sababu iliyotolewa ya kuondolewa kwake kuwa si mzabuni aliyepewa alama ya chini zaidi kifedha, ilikiuka masharti yaliyowekwa katika nyaraka ya zabuni. Mlalamikaji alisisitiza kuwa zabuni ilitumia njia ya QCBS, ambayo inamaanisha kuwa bei haikuwa kigezo pekee cha kuzingatia, bali wazabuni pia walitakiwa kupimwa kulingana na uzingatiaji wao wa vigezo vya kiufundi. Hata hivyo, kinyume na sheria, kanuni, na njia ya QCBS, wakati wa kutathmini zabuni, Wizara ilizingatia tu bei zilizotolewa.

Kwa upande mwingine, Wizara ilipinga hoja ya mlalamikaji kuwa mchakato wa tathmini ulifanyika kwa mujibu wa nyaraka ya zabuni, Sheria na Kanuni zake. Ilisisitiza kuwa baada ya kumaliza mchakato wa tathmini, mlalamikaji alipangwa nafasi ya tatu na hivyo hakupewa zabuni kwa kuwa alishika nafasi ya tatu. Aidha, Wizara ilieleza kuwa wakati wa kutoa taarifa ya kusudio la kutoa zabuni (Notice of Intention to Award), mfumo wa NeST ulitengeneza sababu tofauti ya kuondolewa kwa mlalamikaji, tofauti na hitimisho la taarifa iliyopo katika ripoti ya tathmini.

Mamlaka ya Rufani pia ilikagua taarifa ya kusudio la kutoa zabuni na kubaini kuwa mlalamikaji aliondolewa kwa sababu hakuwa mzabuni aliyewasilisha zabuni yenye bei ya chini zaidi ya kifedha. PPAA iliangalia uchambuzi wa tathmini na kubaini kuwa baada ya kumalizika kwa mchakato wa tathmini, mlalamikaji alipangwa nafasi ya tatu na kwa hivyo hakustahili kupewa zabuni. Kwa kuzingatia hali hiyo, ni wazi kwamba mlalamikaji aliondolewa kwa haki, ingawa taarifa ya kusudio la kutoa zabuni ilitoa sababu tofauti ya kuondolewa kwake. Kwa msingi huo, PPAA ilikubaliana na hoja ya mlalamikaji katika jambo hili. Hata hivyo, kwa kuwa mlalamikaji aliondolewa kwa haki, PPAA iliikumbusha Wizara ya Mawasiliano kuwa makini wakati wa kutoa taarifa ya kusudio la kutoa zabuni, ili kuhakikisha kuwa inatoa sababu halisi za kuondolewa kwa mzabuni kama zilivyoainishwa kwenye ripoti ya tathmini.

Kuhusu msingi wa tatu wa rufaa wa mlalamikaji unaodai kuwa hakupokea matokeo ya tathmini ya mapendekezo ya kiufundi, Mamlaka ya Rufani ilibaini kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma inataka washauri ambao wamepata alama za juu ya kile kiwango kilichoainishwa kwenye kabrasha la zabuni kufahamishwa tarehe na mahali pa ufunguaji wa mapendekezo ya kifedha.

Kwa kuzingatia hali hiyo, PPAA ilifikia uamuzi kuwa Wizara ilitakiwa kumjulisha mlalamikaji kuwa alipata alama za juu zaidi ya kiwango kilichoainishwa na kumpatia taarifa ya tarehe ya ufunguaji wa mapendekezo ya kifedha. Aidha, Mamlaka ya Rufani iliona kuwa kwa kuwa taarifa hiyo haiwezi kutolewa kupitia mfumo wa NeST, kama ilivyodaiwa na Wizara, basi ilikuwa jukumu la wizara kuhakikisha kuwa taarifa hiyo inatolewa ili kuzingatia masharti ya Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Kulingana na matokeo hayo, mlalamikaji hakupewa sifa ya kushinda zabuni kwa kuwa alipangwa nafasi ya tatu; kwa hivyo kuondolewa kwake kulikuwa na msingi. Hivyo, PPAA imetupilia mbali rufaa ya Mlalamikaji kwa kukosa mashiko na kuiruhusu Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia sheria.

# HABARIPICHA




*Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda hilo kwenye Maonesho ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni, Agosti, 2025 jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Bw. Jacob Kibona akimsikiliza Mkuu wa Sehemu ya Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) Bi. Agnes Sayi alipotembelea banda la PPAA katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, Julai 2025 jijini Dar es Salaam.*




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA), Profesa Geraldine Rashel akizungumza na watumishi wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) alipotembelea banda la mamlaka hiyo kwenye Maonesho ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Waziri Mkuu Mstaafu John Malecela, Nzuguni, Agosti 2025 jijini Dodoma.*

# HABARIPICHA

*Ujumbe kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ukiongozwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Mhe. Awadh Bawazir ukibadilishana uzoefu kuhusu ukaguzi katika sekta ya ununuzi na ugavi katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Kosovo wakati ujumbe wa PPAA ulipofanya ziara ya kubadilishana uzoefu Julai 2025 jijini Prishtina, Kosovo.*





*Ujumbe wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ukiongozwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Mhe. Awadh Bawazir (aliyesimama katikati) katika picha ya pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Kosovo Bi. Vlora Spanca (aliyevaa nguo nyeupe) wakati ujumbe wa PPAA ulipofanya ziara ya kubadilishana uzoefu katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Kosovo Julai 2025 jijini Prishtina, Kosovo.*

# HABARIPICHA



*Ujumbe wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ukiongozwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Rufani, Jaji Mstaafu Mhe. Awadh Bawazir ukizungumza kuhusu ununuzi wa umma na Manispaa ya Jiji la Prishtina wakati ujumbe wa PPAA ulipofanya ziara ya kubadilishana uzoefu wa matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa Kieletroniki, Julai 2025 jijini Prishtina, Kosovo.*




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na watumishi wa Wizara ya Fedha alipowatembelea katika banda la wizara hiyo kwenye Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba, Julai 2025 jijini Dar es Salaam.*



*Ujumbe kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), katika picha ya pamoja na ujumbe kutoka Tume ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRC) baada ya kubadilishana uzoefu kuhusu matumizi ya Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa Kieletroniki, Julai 2025 jijini Prishtina, Kosovo.*